

2.6. Udhhibiti wa Maonesho yote ya kimataifa nchini

Kusimamia Ubora na Viwango vya Maonesho ya biashara yote ya kimataifa yanayofanyika nchini.

2.7 Ushauri juu ya Sera za Biashara na Uwezesaji

Kuishauri Serikali kwenye masuala ya uundaji, uendeshaji, usimamizi, utekelezaji na uboreshaji wa sera ya biashara pamoja na mikakati na masuala mengine yahasuyo biashara.

2.8 Urajimu (Branding) wa Bidhaa na Huduma za Tanzania

Kuratibu kuanzishwa kwa rajamu (Brands) na kauli mbiu ya bidhaa na huduma za Tanzania na kuzitangaza katika soko la ndani na nje ya nchi.

2.9 Huduma za Ushauri juu ya Ushindani wa Kibiashara

Kutoa ushauri juu ya Ushindani wa kibiashara kwa Wazalishaji, Wafanyabiashara na Wadau mbalimbali ili kuweza kufikia mahitaji, vigezo, viwango na Ubora wa masoko ya ndani na kimataifa.

WASILIANA NASI KUPITIA

Mkurugenzi Mkuu,

Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania,

Uwanja wa Maonesho wa Mwl. J. K. Nyerere,
Barabara ya Kilwa,

S.L.P 5402, Dar es Salaam, Tanzania.

Simu. +255-22-2850 238,


Nukushi +255-22-2850239/539.

Barua pepe: info@tantrade.or.tz

Tovuti: www.tantrade.or.tz



“Tunaunganisha
Uzalishaji na Masoko”



1.0 UTANGULIZI

Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) ilianzishwa na Sheria ya Bunge Na. 4 ya mwaka 2009 na kuanza shughuli zake rasmi tarehe 3 Septemba, 2010 (GN Na 338). Uanzishwaji wake ulitokana na kufutwa kwa Sheria ya Bunge Na. 15 ya 1973 iliyoanzisha Bodi ya Biashara ya Ndani (BIT) na Sheria ya Bunge Na. 5 ya 1978 iliyoanzisha Bodi ya Biashara ya Nje (BET). TanTrade ni chombo cha serikali chenye mamlaka ya udhibiti, utendaji, na ushauri wa kuendeleza na kukuza biashara ya ndani na nje ya nchi.

1.1 DIRA

“Kuwa kitovu cha ufanisi wa hadhi ya kimataifa katika kuendeleza na kukuza uchumi wa nchi kupitia biashara”

1.2 DHIMA

“Kuwezesha ukuaji wa uchumi wa Tanzania kupitia kuendeleza na kukuza bidhaa na huduma mbalimbali kwa masoko ya ndani na nje ya nchi”

1.3 VIINI THAMANI

- Utaalamu katika utoaji huduma
- Utekelezaji wa majukumu kwa ushirikiano
- Uadilifu, Utawala bora, Uwajibikaji na Uwazi
- Ushiriki katika masuala ya kijamii

2.0 HUDUMA ZA SHIRIKA

Shirika linatoa huduma mbalimbali kama ifuatavyo:

2.1 Huduma za Taarifa za Biashara.

Kukusanya, kuchambua, kuhifadhi na kutoa taarifa mbalimbali za biashara kwa jamii ya wafanyabiashara na wadau mbalimbali.

2.2 Kuwajengea Uwezo na Kuwaendeleza Wazalishaji (Wajasiriamali) Wadogo

Kutekeleza programu mbalimbali za kuwajengea uwezo wajasiriamali kwa kutoa mafunzo, kliniki za biashara, na huduma za ushauri kwa jamii ya wafanyabishara na hasa kipaumbele kikiwekwa kwa wazalishaji wadogo ili waweze kushindana katika masoko ya ndani, Kanda na Kimataifa.

2.3 Ukuzaji wa Bidhaa na Huduma za Tanzania

Tunakuza bidhaa na huduma kwa:

- Kuandaa Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF) pamoja na Maonesho mengine ya kisekta naye Kanda zote nchini.
- Kuratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Maonesho ya dunia, misafara ya Biashara na mikutano ya wafanyabiashara.

2.4 Utafiti na Maendeleo ya Masoko

Kufanya tafiti mbalimbali za kibiashara, udadisi wa masoko na maendeleo ya masoko. Ili kutambua changamoto, mahitaji, mienendo ya masoko, fursa na kuongeza thamani.

2.5 Kuendeleza Bidhaa na Masoko ya ndani

Kutambua bidhaa zenye fursa katika masoko na kuendeleza kwa kuyaongezea ongezeko la thamani, na kuratibu maendeleo ya mifumo ya masoko ya ndani na kuhakikisha kuwa biashara ya ndani inaunganishwa na biashara ya nje.